

MAENDELEO YA BIDHAA KATIKA KITUO CHA MAFUNZO YA VIWANDA VYA MAZAO YA MISITU NA MBAO

Taarifa za jumla

- Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazao ya Misitu na Mbao (FWITC) kinahudumia mnyororo thamani wa msitu si kwa mafunzo tu, bali pia kwa kutoa huduma za maendeleo ya bidhaa.
- Kwa sasa kituo kinaunda boti zilizoboreshwa kwa ajili ya wavuvi wa Nyasa. Mchakato wa maendeleo ulianza Novemba 2017 na utamaliza wakati wa 2018. Hatua za maboresho zilianza mwezi November 2017 na zitamalizika ndani ya mwaka 2018.
- Boti hizi mpya zinatengenezwa kwa ushirikiano wa mradi pamoja na wavuvi wa Nyasa walioomba kituo kiwatengenezee aina mpya kwa ajili yao.
- Mambo ya msingi yaliyozingatiwa wakati wakutengeneza boti hizi mpya ni pamoja na usalama wa uendeshaji chombo, unafuu wa gharama za uundaji, urahisi wa kutumia na gharama za chini za matengenezo.
- Boti mpya zinategemewa kuongeza kiwango cha uvuvi kutokana na hai yake ya uzito mdogo pamoja na kupakwa koti vizuri ambayo itawaongezea wavuvi ufanisi na kuwapa mazingira salama ya uendeshaji, kwakuwa boti mpya haziingizi maji na ni rahisi kuongoza
- Tazama picha kulia ili kuona boti mpya na ya zamani nyuma.




Vipimo na gharama za ujenzi

- Mpaka sana aina mbiali za boti zimeshatengenezwa. Boti zote mbili ni kwa lengo la uvvia. Boti ndogo ni kwa ajili ya watu 2 pamoja na mzigo wa kilo 100 wakati boti kubwa inauwezo wa kubeba watu 6 na na mzigo wa kilo 200.
- Boti ndogo inaurefu wa meta 4.7 ikiwa na bimu 1.2 meters.
- Boti kubwa inaurefu wa meta 7.2 na bimu ya 1.2 meters.
- Gharama za jumla za ujenzi wa boti inakadiriwa kuwa nusu milioni kwa boti ndogo na milioni kwa boti kubwa. Mchanganuo unaweza kuonekana hapa chini.

Malighafi na gharama za boti ndogo

kipengele	Malighafi	Gharama
Malighafi za kuundia	Plaiwood , mbao zilizorandwa	229,000TSH
Malighafi ya kupaka	Gundi ya kuzibia, wavu wa faiba, rangi ya vya majini, rangi ya mbao za majini	226,300TSH
Malighafi nyingine za kuundia	Kikazio, skurubu ya mbao	17,500TSH
Jumla ya gharama za kuunda	470,000TSH	
Matengenezo yanayohitjika	Msasa na rangi kupaka ya kuanzia	10,000TSH
Makadirio ya mzunguko wa matengenezo	Miaka 3	
Makadirio ya maisha yake	Miaka 10	



Malighafi na gharama za boti kubwa

kipengele	Malighafi	Gharama
Malighafi za kuundia	Plaiwudi , mbao zilizorandwa	405,000TSH
Malighafi ya kupaka	Gundi ya kuzibia, wavu wa faiba, rangi ya vya majini, rangi ya mbao za majini	399,000TSH
Malighafi nyingine za kuundia	Kikazio, skurubu ya mbao	200,000TSH
Jumla ya gharama za kuunda	1,004,000TSH	
Matengenezo yanayohitjika	Msasa na rangi kupaka ya kuanzia	40,000TSH
Makadirio ya mzunguko wa matengenezo	Miaka 3	
Makadirio ya maisha yake	Miaka 20	



Huduma za utengenezaji bidhaa

- Huduma za ushauri wa nbidhaa na hatua za utengenezaji zinazoweza kufanyika kituoni au sehemu husika zinapotengenezwa.
- Mpango biashara na huduma za ushauri zinaoweza kufanyika sehemu husika au kituoni.
- Kupima sampuli za mbao
- Maelezo ya mashine

Kituo kinatoa msaada wa uagizwaji wa mashine, kuunganisha wadau na kutafuta fedha za kusaidia uwekezaji. Kituo kinaweza kutumiwa pia kuandaa warsha, matukio na mikutano ya wateja.

Mawasiliano na namna ya kufika kituoni

Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazao ya Misitu (KMVMM)
Kinyanambo
Mafinga

Mr. Edigary, Mwaifweya Meneja wa Kituo.
Barua pepe: edigary.mwaifweya@privateforestry.or.tz
Tel: +255 744 874 521

Maelezo kwa watumiaji magari: Njia panda ya kituo cha Mafuta cha CF, barabara iendayo Madibira, endesha umbaki wa kilomita moja. Utaona kibao cha kituo upande wa kushoto mwa barabara, mkabala na kiwanda cha mkaa.

Kuhusu Programu ya Panda Miti Kibiashara PFP

Pandamiti Kibiashara husaidia umiliki binafsi wa mashamba ya miti hasa katika uanzishwaji na utunzaji wa mashamba ya miti kwa wakulima wadogo, kadhalika viwanda vya mazao ya misitu pamoja na ukuaji wa soko la mazao ya mbao yaliyokomaa ambayo yatanufaisha wadau wote. Programu inatekeleza katika Mikoa minne: Iringa, Njombe, Morogoro na Ruvuma.

Mradi unafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finland na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania